Sura Za Kristo

Hilo ni tamu sana kwako, kusema hivyo.

Nina furaha sana kuwa katika nyumba ya Bwana. Kuna mahali pamoja tu bora zaidi, na hapo ni kuwa pamoja na Bwana. Sivyo? Wakati ni . . . Taabu zote na majaribu na shida za maisha zitaunganika katika kesho kuu, tukufu. Na bila shaka tunatazamia wakati tutakapomwona.

2 Basi mtu fulani alikuwa akiniuliza, hivi majuzi, akasema, "Unafikiri, Ndugu Branham, ya kwamba Kuja kwa Bwana kumekaribia?"

Nikasema, "Bila shaka ninaamini."

Kasema, "Vema, nimelisikia kwa muda mrefu."

3 "Lakini," nikasema, "siku moja utalisikia kwa mara ya mwisho." Mnaona? Hiyo ni kweli, kwa sababu Yeye—Yeye atawasili siku moja. Na hata iwe ni lini, nataka tu kuwa tayari. Mimi . . . hiyo ni . . .

4 Tulikuwa tunazungumza, hivi majuzi, mbele ya wafanyabiashara fulani, waliokuwa mawakili, na kadhalika. Na—nao wakasema . . . Mmoja akasema, "Lengo la—lako kuu maishani ni lipi?"

Nikasema, "Nina moja."

Akasema, "Ni lipi hilo?"

5 Nikasema, "Kuwaokoa watu kwa ajili ya Kristo." Hilo ndi—ndilo jambo pekee ambalo mimi . . .

6 Shauku yangu kuu zaidi, na shauku ya pekee, ni kumwona Yesu Kristo ametukuzwa. Ninaliishia hilo.

7 Nami nina furaha sana, ushuhuda wetu, kwamba miaka thelathini na mmoja inatimia sasa, nimemtumikia kwa unyenyekevu. Kama nikiishi miaka milioni moja, ningalikuwa na maisha kiasi hicho ya kuishi, ningetaka kuishi kila dakika yake kwa ajili Yake. Kwa kuwa mimi . . . Na kama nilijua ningekataliwa mwishoni, ni majaliwa makuu sana kumwishia Yeye! Yeye ni halisi na mzuri sana!

8 Wala sijawahi kupata chochote, katika safari zangu zote za maisha, ambacho kwa njia yoyote kingelinganishwa na ushirika tulio nao pamoja tunapokuwa peke yetu, mimi na Yeye. Hakuna ushirika mtamu zaidi. Ni mkuu kuliko upendo wa chochote, wa mke, watoto, au chochote, ni upendo wa Kristo. Ni mzuri sana.

9 Sasa, tuna furaha sana kuona uamsho huu ukiendelea juma zima. Na kusikia ya kwamba Ndugu Parnell, na wengine, wamekuwa wakitoa hotuba nzuri sana hapa. Nasi tunaamini kwamba kwenye uamsho huu . . .

10 Uamsho wakati mwingine hueleweka vibaya. Mtu anafikiri kwamba uamsho ni kuleta washiriki wapya kanisani. Hapana. Matokeo ya uamsho ni hayo. Lakini uamsho ni kuamsha kile ambacho tayari kiko kanisani. Mnaona? Ni ku—ni kuwaleta hao.

11 Kuna wakati mmoja niliposimama kando ya ufuo wa bahari, nami na—nadhani nimelinukuu mara nyingi, lakini ni . . . ilikuwa muda mrefu, miaka mingi iliyopita. Nayo ilikuwa ni mara ya kwanza niliyopata kuona, vema, haikuwa ni bahari, ilikuwa Ziwa Michigan. Mimi na Hope tulikuwa huko wakati Kongamano la Dunia lilipokuwepo. Hiyo ilikuwa, ninaamini, yapata 1922, Ndugu Egan, vizuri ninavyokumbuka, wakati Kongamano la Ulimwengu lilipokuwa huko—huko Chicago. Ilikuwa ndiyo mara yangu ya kwanza kuona eneo kubwa la maji. Nami nikasimama huko nje siku hiyo, na kuona hayo mawimbi makubwa. Ni kama vile . . . Asubuhi ya Pasaka, walikuwa na ibada ya mapambazuko huko nje. Na kuona hayo mawimbi makubwa yakiingia na kutoka, na, loo, ilionekana kana kwamba yalikuwa na furaha sana.

12 Lakini nikaanza kufikiria, "Unajua, hakuna maji zaidi katika ziwa lile, nalo likiendelea namna hiyo, kuliko ilivyo wakati limetulia kimya. Ni kiasi kile kile cha maji, hamna tone moja zaidi." Lakini nikawazia, "Vema, kwa nini u—upepo unashuka na—na kulitikisa ziwa namna hiyo?" Ni kutoa takataka zote kwenye ziwa. Mnaona? Unatupa takataka yote ufukoni. Wakati . . .

13 Na halafu nawazia, "Hiyo ni kama ziwa kuwa na uamsho." Mnaona? Unalitikisa, na kulirusha-rusha, na kulitikisa huku na huko, mpaka takataka zote zinatoka. Hivyo ndivyo tu uamsho ulivyo, ni kutufanya tuingie katika Roho wa Bwana, na kushangilia, na kusahihisha makosa, na mwendo wa karibu zaidi, na kujitakasa upya, na kujiweka wakfu, mpaka mambo yote na mashaka yote ya ulimwengu yanatupwa nje ukingoni, mnaona. Ndipo ni mtiririko mzuri, safi, tangu hapo na kuendelea, wakati meli ya kale ya maisha inapoanza mwendo kupitia humo. Loo, sio lazima uangalie sana, kwa sababu kila kitu kimeondolewa. Hilo ni zuri.

14 Vema, usiku wa leo, hatutaki kuwaweka muda mrefu kupita kiasi, huu ukiwa ni usiku wa Jumatatu, na usiku wa kwanza wa juma, kwa usiku wetu wa uamsho. Nami nilifurahi sana kutangaza ya kwamba uamsho unaendelea.

15 Nami nina marafiki wengi. Ninaona baadhi ya ndugu hapa, na jamaa ambao wamenipa ndoto ambazo wameziota, katika majuma machache yaliyopita. Naye Bwana amenisaidia kupata tafsiri ya mambo hayo sasa. Sijui ni nani aliye katikati yetu, na ni wageni wangapi, ama chochote zaidi. Lakini Bwana Mungu angali anatoa fasiri za ndoto. Ni halisi na kamili.

16 Naye ni Mungu yeye yule aliyekuwa katika siku za Yusufu, wakati—wakati yule mfalme alipoota zile ndoto. Naye akamfasiria, na ilikuwa ni sahihi. Na baadhi ya ndoto hizo zinadumu hata wa leo. Matokeo yazo bado yanaendelea. Na, Danieli, katika siku za Nebukadreza.

17 Naye maskini mchungaji wetu mtukufu, mnyenyekevu alisema, muda mfupi uliopita, vema, yeye—yeye kamwe hakutaka kuniomba nisaidie zaidi juma hili. Alisema, "Ninajua umechoka, Ndugu Branham. Lakini," kasema, "vema," alisema, "tunasubiri tu na kushangaa." Hilo ni sawa.

18 Jambo lingine, ilinibidi kufutilia mbali mkutano wa Sydney, Australia, kwa sababu wasingenipa visa wakati huu, mnaona, kuondoka Marekani wakati huu. Na, kwa hiyo, na mambo mengine, kwa hiyo siwezi kwenda kwenye wakati huu. Sijui ni lini nitakapoweza kwenda. Lakini hivi karibuni nitaweza. Lakini tulipolazimika kuirudisha nyuma kidogo, ninaenda Chicago sasa, kwenye m—mkutano huko Chicago, unaokuja. Ambao, walikuwa wametangaza kwamba nilikuwa niwe huko, lakini pasipo kunijulisha mimi. Wakati ambao nilipaswa kuwa huko, nilikuwa niwe katika Visiwa vya Fiji, ambako walisema kutakuwa na watu wengi wamekusanyika huko, pia, visiwani. Lakini sitaweza kuuchukua huo mkutano sasa hivi, huko, kwa sababu ya haki za visa. Na, lakini, nitafanya hivyo, karibuni. Wanasubiri tu.

19 Sasa nitakuwa Chicago. Gene, unajua hiyo ni tarehe zipi? Je, kuna mtu anayejua hiyo ilitangazwaje? Hata sijui ilikuwa lini. Ndio kwanza niione katika *Mbiu Ya Imani*. Ninaamini inaanza kwenye tarehe 4 au 5 ya mwezi, au kitu kama hicho. Au, ni hili lijalo, yapata juma moja kutoka sasa, siku kumi. Na kwa hivyo nimekuwa chini ya majaribu mengi, nami nataka maombi yenu.

20 Sasa, usiku wa leo, nimechagua kusomwa kwa Maandiko kadhaa, kama mngependa kusoma pamoja nami, kutoka katika Yohana Mtakatifu mlango wa 13, sehemu tu. Ninyi mnaoziweka Biblia zenu karibu, na mnapenda kufuatilia kusoma, tunaposoma.

21 Na mara baada ya ibada hii, usiku wa leo, kutakuwako na mazoezi ya arusi hapa. Kwa hiyo, mara tu tunapofumukana, naomba tuharakishe sana, tuwezavyo. Sio kuharakisha; lakini mara tu jengo litakapokuwa tupu, basi wanataka kufanya mazoezi ya arusi. Basi kutakuwa na arusi hapa, kesho usiku. Watoto wetu wawili katika ushirika wa maskani hii watafunga ndoa kesho usiku, kama nyote mjuavyo. Ndugu yetu mpendwa, David Wood anaoa, atamwoa Marilyn Jefferies, kesho usiku, maskanini, kabla tu ya zile ibada. Na kwa hivyo arusi hii inapaswa kufanyiwa mazoezi. Ninii tu. . . Haitakuwa rasmi; itakuwa arusi nusu rasmi kesho usiku.

Sasa, kabla hatujalisoma Neno Lake, na tuombe.

22 Baba Mungu, tunapokuja kwa uchaji sana Mbele Zako, tukilitanguliza Jina litoshelezalo kwa yote la Yesu, tumehakikishiwa kwamba utatusikia. Kwa sababu, Yeye alisema, "Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalitimiza." Kwa hiyo, tunakuja, kama Wakristo waaminio, kwa ujasiri kwenye Kiti cha Enzi cha neema, tukijua jambo hili, kwamba, ikiwa mioyo yetu haituhukumu, basi tunajua maombi yetu yamejibiwa na Mungu.

23 Nasi tunaomba kwamba maisha yetu yawe ya kuridhisha sana Kwako, kwa kuyaungama makosa yetu, na haki Yake kutusamehe, ili shauku zetu zitimizwe usiku huu. Pia, Bwana, shauku yetu kuu ni kuona neema Yako kuu ikimwagwa juu yetu, na hiyo ni—ni, kutusamehe dhambi zetu na kuponya maradhi yaliyo katikati yetu. Nawe unaweza kusema nasi kwa njia ya ufunuo, au unabii, au chochote tu ambacho ungetamani kuliambia Kanisa Lako. Mioyo yetu na iwe vipokezi vya Roho Wako. Jalia tuunganishwe sana na ule mkondo mkuu usiku wa leo, Roho Mtakatifu apate kusema na mioyo yetu, na kupata utukufu kutokana na Uwepo Wake.

24 Sasa, Bwana, tungewaombea wote walio wagonjwa na wahitaji. Kwa maana, kabla tu ya kuja, jinsi ambavyo katibu wetu alivyoweka mezani pangu, katika siku mbili zilizopita, safu ndefu tu za majina, kote nchini, wanaoteseka, wanaokufa, dharura zilizoandikwa kwa rangi nyekundu. Nami ninapoweka kidole changu juu ya kila mmoja wao, nikishuka kwenye ukurasa, Ee Mungu, mbele ya kanisa hili, usiku wa leo, ninasihi kwa ajili ya neema na rehema Zako, kwa kila mmoja. Wewe wajua kila mmoja wao, na wanachohitaji.

25 Wala hatutawasahau wale, Bwana, ambao wanapata ahueni, usiku wa leo, walio huko katika nyumba za wazee na wasiojiweza. Ee Bwana Mungu, wengi wa hao ni watoto Wako waliooshwa kwa Damu. Loo, tunapozeeka, na wapendwa wetu wamesahau, kuna faraja moja tuliyo nayo: Mungu kamwe hasahau. Matendo yetu yote yameandikwa kwenye Kitabu cha Uzima, na milele yako Mbele Zake. Nasi twawaombea, usiku wa leo, Bwana.

26 Tunaomba rehema kwa taifa letu. Na kwa wale wanaotenda dhambi na kufanya maovu, na kwa wale walio kwenye vyumba vya pombe na—na katika maeneo mbalimbali ya dhambi, usiku wa leo, tungeomba neema ya kusamehe, Bwana. Nasi tunaomba ya kwamba utatutegemeza sana, Bwana, hata mioyo yetu itajaa sana upendo kwa ajili Yako, hata itakuwa ni shauku yetu kuu kukutumikia Wewe na kuwaona hao wakiokolewa.

27 Bariki kusomwa kwa Neno, na yote tufanyayo. Kwa unyenyekevu tutainamisha vichwa vyetu na kukushukuru Wewe, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

28 Sasa fungueni Kitabu cha Yohana Mtakatifu, mlango wa 13, tutasoma kwa sehemu.

> *Basi kabla ya sikukuu ya Pasaka, Yesu, hali akijua ya kuwa saa yake imefika, atakayotoka katika ulimwengu kwenda kwa Baba, naye ali amewapenda watu wake katika ulimwengu, aliwapenda upeo.*
>
> *Hata wakati wa chakula cha jioni, naye Ibilisi* sasa amekwisha *kumtia Yuda Iskariote, mwana wa Simoni, moyo wa kumsaliti;*
>
> *Yesu, hali akijua ya kuwa Baba amempa vyote mikononi mwake, na ya kuwa alitoka kwa Mungu, naye anakwenda kwa Mungu;*
>
> *Aliondoka chakulani, akaweka kando mavazi yake; akatwaa kitambaa, akajifunga kiunoni.*
>
> *Kisha* akatia *maji katika bakuli,* akaanza *kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuifuta kwa kile kitambaa alichojifunga.*
>
> *Hivyo yuaja* kwa *Simoni Petro: naye Petro akamwambia, Bwana, wewe waniosha miguu mimi?*
>
> *Yesu akajibu, akamwambia, Nifanyalo* sasa *wewe hujui. . . lakini utalifahamu baadaye.*

29 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye usomaji Wake, wa Neno. Nataka kuchukua so—somo, usiku wa leo, kwa muda mfupi tu, somo la: *Sura Za Kristo*. Nami ninataka, kwa ajili ya somo, "Hii ingekuwa nini? Kinahitaji nini kumfanya Mkristo?"

30 Sasa, najua hili, kwa jumla, si somo la kiinjilisti, la hasha. Na, hata hivyo, ni somo la kiinjilisti, kwa sababu Kanisa haliwezi kamwe kuendelea mpaka lijue linaendelea kwa misingi gani.

31 Nami ninaamini kwamba kabla mtu yeyote hajaweza kutenda kazi ama kupata imani halisi yenye matumaini, ni, kwanza, wanapaswa kujua mahali wanaposimama, na jinsi ya kusimama baada ya kuchukua msimamo wao. Naamini hilo ni muhimu. Kwa maana, huwezi kujitumbukiza tu katika jambo fulani bila kufikiria, kwa imani, wakati hujui unakotumbukia. Huna budi kujua. Na ikiwa imani yetu imewekwa sawa, na mahali pafaapo, inaleta utoshelevu thabiti.

32 Ni kama tu vile ilivyosemwa juu ya mwanamke ambaye, labda, wakati ameolewa, kwamba yeye ana—ana hamu sana kumkumbatia mtoto wake mchanga wa kwanza, hata hajui. . . anaweza kungojea. Lakini yeye, ndivyo matarajio yake yalivyo. Lakini, nyuma ya hayo, kuna hofu, kama haionekani upesi, kwamba hatampata mtoto huyu. Basi hiyo inamsukuma mbali zaidi, wakati wote.

33 Sasa, kuna tiba wanayotumia siku hizi, nayo imetumika katika nyakati zote, iwapo mwanamke huyo anaona au anaamini

kwamba hatamzaa mtoto huyu. Kama atatoka tu na kumwasili mtoto, basi, muda si muda mwajua, atapata wake mwenyewe. Sasa, hiyo imethibitishwa kuwa ni kweli, mara tisa kati ya kumi. Kwa sababu mkazo huo wa kushangaa, "Loo, labda sitampata." Lakini hilo linahitaji utoshelevu huo mdogo pale, nayo labda ni njia ya Mungu ya kumweka katika hali inayofaa. Ndipo atampata mtoto wake mwenyewe, kwa sababu hofu hiyo na matarajio hatimaye yatamwacha.

34 Ndivyo ilivyo kwa watu wanaotaka kuponywa, wao, kama wanaweza kuwa na ushahidi mmoja mdogo tu unaoonekana.

35 Kama vile Eliya, aliposema . . . Gehazi aliposema, "Ninaona wingu dogo kama mkono wa mtu."

36 Eliya anasema, "Nasikia sauti ya mvua tele." Aliona ushahidi.

37 Hiyo ndiyo sababu, mara nyingi, nawaambia watu, "Endeleeni, anzeni kumsifu Bwana." Mnaona? Kwa sababu, huyo ndiye mtoto aliyeasiliwa, maana liko akilini mwao mpaka litakapoingia nafsini mwao, kwamba wameponywa, ndipo imani inalifanya kweli.

38 Unapaswa kujua unachofanya. Unapaswa kuwa na imani katika yale ufanyayo.

39 Kwa hivyo, mara nyingi sana, tunasikia usemi huu, "Loo, Mkristo ni nini?"

40 Baadhi ya watu wanaiwekea mpaka kwenye kujiunga na kanisa. Mtu fulani alisema, "Vema, Mkristo ni m—mfuasi wa kanisa, mtu anayejishirikisha na kanisa." Ninaamini kwamba Wakristo wote wanapaswa kufanya hivyo, bali siamini huo ndio Ukristo. Mnaona? Hivyo ndivyo Mkristo anavyofanya akiisha kuwa Mkristo. Ila haimaanishi, kwamba, kwa sababu anafanya hivyo, kwamba yeye ni Mkristo.

41 Kisha wengine wanasema, "Hapana. Ni kwenda kanisani na kutumikia azimio la kanuni za imani, na kuwa mwaminifu kwa yale mambo ambayo kanisa hufundisha."

42 Halafu wapo wengine wanaosema, kwamba, "Labda ni kubeba maskini—maskini kitu fulani, m—msalaba mdogo ama chochote kile, kwamba hiyo ndiyo ishara ya Mkristo."

43 Vema, halafu kuna wengine wanaoamini, kwamba, "Huenda ikawa, labda, kama wangeweza kuwasha mshumaa, au kufanya namna fulani ya kitubio, kwamba huyo ni Mkristo. Ikiwa watazamishwa tu majini, au watatoa sadaka, au kulipa kanisa kitu fulani, au—au kumsaidia jirani, kumnunulia mjane makaa, au viatu kwa yatima." Hayo ndiyo matendo ambayo Mkristo anapaswa kufanya, lakini hilo bado haliwafanyi kuwa Mkristo.

44 Halafu wengine wanasema, ya kwamba, "Ukiweka sanamu ya Kristo kwenye gari lako, au kwenye ukuta wako, kwamba

hiyo ni ishara ya Mkristo." Vema, mambo hayo ni sawa, ila siamini ya kwamba kubeba sanamu kunakufanya Mkristo.

45 Ninaamini ya kwamba kuwa mfano wa Kristo kunakufanya kuwa Mkristo. Sio kile tufanyacho, kwa nje. Ni kile kilichotukia, kwa ndani, ndicho kinachotufanya kile tulicho. Basi, kwa hiyo, ikiwa Yeye ni mfano wetu, nasi tuko katika sura Yake na viungo vya Mwili Wake, tunapaswa kuwa sura kama Yeye. Basi maisha yetu yanapaswa kuakisi sura ya Kristo, si katika kujiunga kwetu na kanisa, au katika kubeba kwetu msalaba, ama mihemko yetu, bali inapaswa kuwa katika Uwepo ulio hai wa Mungu aliye hai ambao unaakisiwa kupitia maisha yetu.

46 Nimeambiwa, na mabingwa, kwamba . . . kabla hawajakuwa na siku za kiyeyushi, kutoa ma—takataka katika dhahabu, kutoa chuma na kimbwi. Kimbwi inafanana sana, na dhahabu halisi, hata inaitwa "dhahabu ya mjinga." Lakini jinsi walivyotoa hayo yote, waliipiga kwa nyundo. Wahindi walikuwa wakifanya hivyo. Na wafua dhahabu wa kale walikuwa wakifanya hivyo, kuipiga kwa nyundo, na kuigeuza tena na tena, na kuipiga mpaka takataka yote ikatoka ndani yake. Na njia pekee waliyojua ya kwamba ilikuwa imebaki tu dhahabu, ilikuwa ni wakati mpigaji aliweza kuona uakisi wake ndani yake. Yule ambaye alikuwa akipiga angeweza kuendelea kutazama, hadi karibu aweze kujinyoa, kwa uakisi wake katika dhahabu aliyokuwa akipiga.

47 Basi Roho Mtakatifu wa Mungu anapoanza kutupiga, kwa nyundo ya Injili, mpaka mambo yote ya ulimwengu yametolewa, nasi tunaweza kuakisi sura ya Bwana Mungu, ndipo ninaamini tunakuwa Wakristo. Maana, neno *Mkristo* linamaanisha "kama Kristo, na kumwakisi Yeye."

48 Sasa hiyo haimaanishi kwamba tunapaswa kufuga ndevu ndefu, kama wasanii wanavyomchora kuwa nazo. Na wala haimaanishi kwamba tukuze nywele ndefu, kama wasanii wanavyomchora kuwa nazo, ama kuvaa joho kama alilovaa, kwa maana tunaishi katika siku nyingine. Si lazima tuwe hivyo, ili kuakisi sura Yake ya kimwili.

49 Lakini ni lazima, nafsini mwetu, tuiakisi sura ya Roho Wake na namna ya maisha Yake. Siamini kwamba Wakristo ni wa kujiunga na makanisa au kanuni za imani. Ninaamini ni uakisi wa Yesu Kristo katika mwanadamu, kwa maana sisi ni washiriki Wake, washiriki wa Mwili Wake, nasi tunauchukua mfano Wake, Maandiko yanasema.

50 Sasa, Yeye alikuwa na mfano wa aina gani? Hakuja kuwa mtu fulani mkuu; hata hivyo, alikuwa ni mkuu. Lakini alikuja kama mtumishi. Hakuja kutumikiwa, bali kutumika. Somo letu, usiku wa leo, linaakisi kile Yeye alichokuwa. Hicho ndicho kinachomfanya kuwa mkuu, katika makadirio yangu. Hata hivyo, akiwa ndiye Mungu wa Milele hasa, Mungu Yule yule

aliyeziumba mbingu na nchi; ndipo alipokuja hapa, alichukua nafasi ya chini kabisa, kazi isiyotamanika kabisa ambayo mtu yeyote angeweza kuwa nayo, hiyo ilikuwa ya mtumishi mwosha miguu.

51 Katika malipo yote, ya siku za mwanzoni, katika ulimwengu wa Mashariki, mtumishi mwosha miguu alikuwa ndiye mwenye mshahara mdogo kuliko wote. Kwa maana, katika siku hizo wanyama walitembea kwenye barabara kuu, zile, njia za kando walizopitia. Basi barabarani, kulinuka, kote barabarani, ambapo wanyama walikuwa. Nayo mavumbi yakaruka juu na kuifunika miguu yao na nyayo zao. Na uvundo mbaya sana, ukatokea! Basi mara tu mtu alipokuja kumtembelea mwingine, hangeweza kuingia kwa namna hiyo. Alinuka vibaya, kutokana na uvundo wa barabarani, na mavumbi, kama kwenye ba—banda la farasi wa kukodiwa.

52 Kwa hiyo, jambo la kwanza alilofanya, alikuwa na kibanda kidogo, kibanda cha mapokezi, na mtu mwenye mshahara mdogo zaidi mahali hapo, kama vile tu mtumwa fulani, alikaa huko nyuma, apate kuosha miguu ya mgeni huyu ajaye, na kumpa jozi nyingine ya viatu avae, maskini ndara, kumvisha. Kisha akapakwa mafuta, na, basi, pamoja na mafuta. Ndipo angeweza kuingia basi kuwa mgeni wa rafiki yake. Maana, angejisikia hafai, kuingia, amejaa uvundo wa ba—barabarani, na jasho, na kadhalika. Naye mtumishi mwosha miguu alipata mshahara wa chini sana kuliko mtu yeyote aliyekuwapo.

53 Naye Mungu wa Mbinguni, akajinyenyekeza, kuwa . . . Yule mkubwa kuliko wote aliyekuwapo akawa wa chini kuliko wote aliyekuwapo.

54 Ni tofauti jinsi gani, ya anayejiita, anayeakisi Mkristo siku hizi! Ni tofauti iliyoje! Mbona, anayejiita Mkristo siku hizi anataka kutumikiwa. Loo, anaanza kuwazia kwamba yeye ni mtu wa maana.

55 Ilikuwa ni tofauti jinsi gani, ilivyokuwa, wakati anapomwakisi Yeye. Kamwe Yeye hakuja kutumikiwa. Lakini Yeye . . . Yeye alikuja kutumika. "Aliye mkubwa kwenu na awe mtumishi wa hao wote."

56 Nasi tumeona, siku hizi, kwamba mwelekeo wetu wa kisasa wa Ukristo ni, "Mimi ni mtu wa maana, na wewe si kitu." Loo, ni . . . Ni makosa. Haipaswi kuwa hivyo. Tunajaribu kuuakisi Ukristo kwa njia mbaya. Mungu hataki tufanye hivyo. Yeye . . . Tuliimba wimbo, *Kuwa Kama Yesu*, lakini inapofikia kunyenyekeza kiburi chetu, na kushuka chini kama Yeye alivyofanya, basi tunaweka mpaka.

57 Na katika kufanya hivyo, mwanadamu amejiundia madhehebu, wapate kujitenga, "inaonekana hawana Roho," kama Maandiko yalivyosema. Wanajitenga. "Sisi ni wa kanisa *fulani-fulani*. Ni—ni kanisa kubwa zaidi. Ni kanisa bora zaidi.

Dhehebu letu ni dhehebu kubwa zaidi." Hilo halitendi kama Yesu. Hilo haliakisi upendo Wake na utu Wake.

58 Alikuja kwa walio duni kabisa, kwa kahaba wa mitaani, kwa mwombaji, kwa lofa, na kushuka moja kwa moja mavumbini pamoja nao. Hayo ndiyo maisha ya Kikristo. Hivyo ndivyo yanavyopaswa kuwa, kumwakisi kwa njia hiyo.

59 Loo, najua watu husema, "Si—siku hizo zimepita." Hazijapita.

60 Ikiwa Kristo angali ni Kristo, ikiwa Roho Wake angali ni yule Roho Mtakatifu aliyekuwa ndani Yake, akiwa ndani yako, atakufanya uchukue msimamo huo, pia.

61 Lakini, siku hizi, tunajaribu kuwazia kwamba sisi ni tofauti. Ni mbali kiasi gani na maombi Yake, hapo alipoomba, kwamba, "Hivi watu wote wangejua kwamba tulikuwa wanafunzi Wake, tunapopendana."

62 Na badala ya hayo, tunazozana. Tunadharauliana, kwa sababu hatukubaliani juu ya mambo fulani. Kisha tunatoka nje na—na kushtakiana, mnaona, ambapo . . . na hata hivyo tunadai kuwa Wakristo. Najua watu wanaodai kuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu, wana hatia ya mambo kama hayo, kutoka nje na—na kusema mambo maovu kweli juu ya Wakristo wengine. Wakati, haiwapasi kufanya mambo hayo. Sasa, ndugu, dada, tunapokuwa na roho ya namna hiyo, afadhali tuweke niani mwetu ya kwamba sisi si Wakristo bado. Haijalishi tunakiri kiasi gani, ni kile tulicho nacho ndicho kinachojalisha. Mnaona? Hatuwezi kuwa Wakristo na tusiwapende watu wote. Tunaweza kutofautiana na watu.

63 Lakini, Yesu hakuweka na kusema, "Vema, sasa, hapa, ninyi Mafarisayo wote, nyote mnaelekea kuzimu. Wala hakuna nafasi kwenu, kwa sababu ya *hili, lile*, ama lile *lingine*, kwa sababu wewe ni Mfarisayo." Lakini aliwaendea, akawahudumia, na kuwasaidia. Alifanya kila aliloweza, kuwasaidia.

64 Lakini, siku hizi, elimu, na ufuasi wa kanisa, na vifungo vya ulimwengu vimelileta kanisa pamoja hivi kwamba mambo ya kiakili yamechukua mahali pa ya kiroho.

65 Huwezi kumfikia Mungu ila kwa Roho. Kuna njia moja tu ambayo mtu anaweza kumjia Mungu, na hiyo ni kwa Roho Mtakatifu. Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba, kwanza." Hiyo ni kweli tu iwezavyo kuwa, Mkristo.

66 Tunataka kuchukua kijitabu kidogo, usiku wa leo, moyoni mwetu, na kuhesabu mambo haya sasa. Hebu tuliwazie hili.

67 Loo, baadhi yetu tunadai kuwa na maarifa yote. Tunao wale wanaosema, "Sasa ngoja!" Wanapenda kuwa "madaktari" na "baba watakatifu," na kadhalika. Lakini ukijua haya yote, kama ulikuwa na maarifa yote, haingekufaa kitu isipokuwa

(ulikuwa) ulikuwa na Roho ndani yako, ya upendo. Biblia ilisema, “Nijapokuwa na maarifa yote, wala sina upendo, si kitu mimi.”

68 Nayo maarifa yetu yana faida gani, mtu anaposema, “Nisingeenda kwenye uamsho kama huo, kwa sababu hao si watu wenye elimu. Ni—nisingeshirikiana nao”?

69 Haidhuru kama hawajui ABC zao, ama la, wanaweza kumjua Kristo. Bila shaka huwezi kushuka kupita kiasi. Mungu na amweke Roho huyo ndani yangu daima. Haijalishi ni—ni duni jinsi gani, anachoamini, asichoamini, ni kanuni gani ya imani, rangi, ama nini, ninataka kunyoosha mkono na kumsaidia. Hakika. Ninamtaka Roho huyo ndani yangu. Sitawazia mimi ni bora kuliko mtu mwingine; ningeweza kuweka kifua changu mbele, na kusema, “Watu wote husimama ninapoingia,” au, “Nina uamsho mkubwa kuliko hao wote.” Mimi ni nani, kwa vyovyote vile, ila udongo ambao Mungu ameufanya? Hebu nijinyenyekeze, maisha Yake yapate kuakisiwa. Hebu, Wakristo wote, tujisikie hivyo. Maarifa hayatufikishi popote.

70 Kwa mfano, vipi kama kuna kizimba kilichojaa kurumbizi, nacho hicho kizimba ni kikubwa kama maskani hii? Ndipo maskini kurumbizi mmoja aruke ndani ya hicho kizimba, na kusema, “Mabwana, nataka kuwaambia ninyi nyote jambo fulani. Inatokea kwamba mimi ni bora kidogo kuliko ninyi nyote. Mnaona, mimi ni—mimi ni kurumbizi anayejua yote kuhusu wanadamu. Loo, naweza kuyaelezea yote. Nimemwona yule mama akitembea kwenye nyumba. Nimewaona watoto wakicheza. Ninajua yote kuyahusu. Sasa ninyi nyote nisikilizeni.”

71 Na yapata wakati anapofoka maneno kutoka bongoni mwake, mwanachuoni wa Chuo kikuu cha Princeton anaingia, mwenye ufasaha kabisa wa lugha. Basi anaanza kuendeleza mazungumzo na maskini kurumbizi huyo, akitumia sarufi ya juu kabisa awezavyo, huku anamzungumzia maskini kurumbizi huyu. Ningewazia maskini jamaa huyo angekigeuza kichwa chake kwa upande. Angesikiliza kutoka upande mmoja hadi mwingine, lakini hajui kitu anachozungumzia. Hata hivyo, anaweza kumsikia. Hata hivyo, anaweza kumwona. Lakini elimu yake inafaa nini? Bure. Kwa sababu, hajui yale huyo mtu anayozungumzia. Kwa nini? Ana ubongo wa kurumbizi. Hana ubongo wa mwanadamu. Anaelewa tu jinsi kurumbizi wanavyoelewa.

72 Basi hivyo ndivyo binadamu alivyo. Sijali una akili kiasi gani. Tungali tuna ubongo wa kurumbizi, kwa sababu sisi ni wanadamu tu. Mungu anajulikana kwa Roho, na kwa ufunuo kwa Roho Mtakatifu. Kamwe hatutaweza kumwelewa kwa elimu. Unaweza kuzungumza, na kuingia na kuwa na mikutano

ya kiakili, na saikolojia kadiri utakavyo, na watu kamwe hawatamjua Mungu. Hawawezi.

73 Unaweza kuelezea na kusema watu wanaolia na kugeuza shavu lingine ni wa mtindo wa kale tu, bali huyo ndiye mtu anayemwakisi Kristo maishani mwake. Mtu aliye mnyenyekevu, mtu atakayetembea pamoja na Mungu, atatenda kama Yesu.

74 Lakini, unaona, huyo maskini ndege asingeweza kuelewa, hata hivyo alidhani angeelewa. Kwa sababu, hajaumbwa hivyo. Akili yake haitalingana na akili ya mwanafunzi huyu mwerevu.

75 Na wala akili zetu kamwe hazitalingana na Mungu kamwe. Maskini akili yetu ndogo, isiyo na kikomo inawezaje kulinganishwa na akili yenye kikomo; au akili yetu yenye kikomo kamwe kulinganishwa na akili isiyo na kikomo ya Mungu? Akili hiyo ya Mungu isiyo na kikomo iko mbali sana na akili za wanadamu hata isingelinganishwa.

76 Njia pekee ambayo ndege huyo atawahi kujua kile huyo mtu anachozungumzia, ni kwa kujitolea mwenyewe na kulikubali, na kufanya chochote anachowazia kwamba huyo mtu anamtaka afanye.

77 Hiyo ndiyo njia pekee ya kumjua Mungu, ni kufuata uongozi wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni ya mtindo wa kale. Ni mpango wa Mungu. Daima imekuwa mpango wa Mungu. Daima itakuwa mpango wa Mungu. "Si kwa nguvu, si kwa uwezo, bali kwa Roho Yangu, asema Bwana." Hapo ndipo inapokujia.

78 Longfellow wakati mmoja alisema hivi, "Njia ya kufanikiwa ni kutafuta hoja inayostahili ambayo inazungumziwa, hoja inayostahili ambayo inazungumziwa, na halafu uishikilie." Hakika. Jambo linalozungumziwa, linalokataliwa na—na sayansi, na, iwapo linafaa, basi lishikilie.

79 Unajua, katika mwaka wa 1872, Shirika la Matibabu la Marekani lilikataa hodhi? Walisema, "Zinakiuka kanuni za afya kabisa." Kisha kasema, "Zitaeneza magonjwa." Hodhi; hatimaye wakazikubalia.

80 Nayo Injili hii ya mtindo wa kale tunayozungumzia, iliyooshwa kwa Damu ya Mwana-Kondoo! Inaweza kuonekana kuwa ya mtindo wa kale, lakini itawabidi kuijia, siku moja. Ni jambo linalofaa. Lishikilie, kwa yote uliyo nayo. Ni njia iliyooshwa kwa Damu ambayo humsafisha mtu; sio kwenda hapa nje, wakinywa pombe na kuvuta sigara, na kukusanyika pamoja na kujiita "Wakristo" kwa sababu wao ni wafuasi wa kanisa. Ni yule Roho Mtakatifu, safi, asiyeghoshiwa katika maisha ya mwanadamu, anayemwakisi Yesu Kristo Mwana wa Mungu.

81 Hiyo ndiyo sababu watu siku hizi wanakataa Kuzaliwa upya. Loo, wana kile wanachoita Kuzaliwa upya, njia ya kupeana mikono na mchungaji, lakini huko si Kuzaliwa. Sababu ya

wao . . . Hawatakukubali. Hiyo ndiyo sababu wanaenda kujiunga na makanisa, kwa sababu wanaweza kuja kwa njia fulani ya kiakili.

82 Mungu alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi hata kuuona Ufalme wa Mungu." Haidhuru una akili jinsi gani, ama unadai kuwa Mkristo mzuri jinsi gani, huna budi kuzaliwa mara ya pili.

83 Unasema, "Basi, Ndugu Branham, itanibidi nije kwenye misheni fulani ndogo?" Hiyo haimaanishi hivyo. Inamaanisha unapaswa kupokea Kuzaliwa upya. Huna budi kuzaliwa mara ya pili.

84 Hili ni kusanyiko lililochanganyikana, lakini nitasema kitu fulani. Kuzaliwa ni nini? Kama kuzaliwa kukifanyika kwenye godoro la majani makavu, au kukifanyika sakafuni, ama katika hospitali ambayo vyumba vimenakshiwa katika hariri ya waridi, ni mchafuko, vyovyote unavyokuchukua. Hiyo ni kweli.

85 Vivyo hivyo na Kuzaliwa upya. Ni mchafuko, vyovyote unavyokuchukua, bali kunaleta Uhai. Amina. Kunaleta Uhai. Uhai wa aina gani? Uhai wa mtumishi, kujinyenyekeza, kujikana. Ni Uhai wa namna hiyo. Loo, wanasema, "Lakini nimewaona wakilia na kudorora madhabahuni na kupiga makelele." Hakika. Wanazaliwa. Ni mchafuko, sijali unaenda wapi. Unaweza kuinuka, uso wako wote umejaa machozi, na macho yako mekundu, na mikono yako imejeruhiwa kwa kupigapiga madhabahuni, lakini ni Kuzaliwa. Kunakufanyia jambo fulani. Kunakufanya mtumishi. Kunakuondolea ugumu. Kunafanya sura, kufinyanga Maisha mapya, kiumbe kipya. Unaweza kuwa umechafuka kabisa, unapoamka, lakini umezaliwa mara ya pili. Haijalishi uko wapi, kunafanya Maisha mapya. Kunaleta Maisha mapya, ya mfano. Kunakufanya mtumishi. Unataka kutumika, basi. Yesu anataka tutumikiane, tu—tupendane. Na tunapotumikiana, tunamtumikia Yeye.

86 Sasa, kumbukeni, wagonjwa pekee ndio wanaohitaji uangalizi, huduma. Wagonjwa tu, wanahitaji uangalizi. Basi unapomwona mhubiri . . . Na hebu nisiiwekee mipaka tu kwa mhubiri, lakini hebu niiweke kwa kila mshiriki wa kanisa ambaye anataka uangalizi, "Mimi ni mtu wa maana," kumbuka tu, huyo hapo mgonjwa wa kiroho. Wanahitaji kushughulikiwa. Wanahitaji kushughulikiwa na Roho wa Mungu, kuwapa kitu kitakachowaondolea mtazamo huo, na kuwaponya kutokana na ubinafsi wao na mawazo yao makubwa, na "mie mkubwa na mdogo wewe." Roho Mtakatifu hutufanya sisi sote kuwa sawa.

87 Ugonjwa mwingi mno wa kiroho, upungufu wa damu! Unajua anemia ni nini? Ni mtu asiye na damu. Wanatembea kigeni. Wao ni shaghalabaghala, ovyoovyo, wakati wote. Na hilo ndilo tatizo la washiriki wetu wengi wa kanisa siku

hizi. Wamepungukiwa na damu. Wanahitaji kupewa Damu, ya Kalvari, ambayo itawapa Damu tajiri, ya kifalme, kuwafanya watembee katika mtindo wa kale, njia ya Mungu iliyochimbwa na Roho Mtakatifu. Ambayo itawapa kitu cha kuishia, kuwapa ujasiri utakaowafanya watembee katika sura ya Bwana wao.

88 Kwangu mimi, kama ningelikuwa na chaguo la kufanya, ninataka liwe kama Yeye alivyokuwa. Alikuja kuwa mchungaji, Naye alikuwa mchungaji. Mchungaji ni yule anayewafuata kondoo wake.

89 Picha maarufu, sidhani kama tunayo kwenye ukuta wetu hapa, lakini nimeketi chumbani mwangu na kuitazama. Siwezi kulikumbuka jina la huyo msanii kwa sasa. Lakini wakati alipompoteza maskini kondoo huyo mweusi, ndipo akawaacha wale tisini na tisa na kwenda kumtafuta, anafanya nini? Anapotelea nyikani. Anajichoma kwa michongoma. Anapitia hatarini. Anawinda usiku kucha. Mpaka, hatimaye, chini kabisa kando ya mlima, akining'inia karibu na kichaka kidogo, akiyahatarisha maisha yake mwenyewe, anaunyosha mkono na kumtwaa maskini jamaa huyo katika hali yake ya kuanguka, kisha anamrudisha kwake.

90 Kisha msanii mwingine akachora picha yake akimleta nyumbani. Sasa, inaonekana kana kwamba huyo mchungaji angeuchomeka tu mkono wake chini ya huyo kondoo, ashike njia kumleta namna *hiyo*. Lakini uliona jinsi roho ilivyoishika brashi ya huyo msanii? Hakumweka chini ya mkono wake. Alimlaza begani mwake. Sasa, nawatakeni mwone uangalizi wa mchungaji huyu.

91 Sasa, Yesu, alipokuwa akiwatoa pepo, Yeye alisema aliwatoa kwa kidole cha Mungu. Sasa, kama ibilisi anakusumbua, kitu tu kinachohitajika, cha Mungu, yeye—yeye ni—hana maana kabisa hata Yeye huchukua tu kidole Chake na kumtoa.

Lakini kondoo anaporudi nyumbani . . .

92 Iko wapi sehemu yenye nguvu zaidi ya mwanaume? Mabegani mwake. Unaona jinsi mtu, sikuzote, mabega yake ndiyo makubwa zaidi? Anaweza kubebea wapi mzigo wake ulio mkubwa zaidi? Mabegani mwake. Ni wapi ambapo ana uhakika kabisa napo? Hapo mzigo unapowekwa mabegani mwake.

93 Kwa hiyo anamchukua huyo kondoo, anamlaza mabegani mwake, na kurudi pamoja naye polepole. Nguvu zote za Mungu, zimezungushiwa jamaa huyo mdogo, aliyepotea, akimrudisha. Lakini ibilisi, rahisi sana, Yeye humtoa tu, kwa kidole Chake. Yeye ni mchungaji.

94 Mchungaji hana budi kutangatanga, ili kumtafuta aliyepotea. Na mchungaji mzuri ni mchunga kondoo. Kusema kweli, ne—neno *mchungaji* maana yake "mchunga kondoo." Na wakati mwingine, kanisani, dhe—dhehebu dogo au kikundi kidogo kitatokea kanisani; upande mmoja utaelekea njia

moja, na upande mmoja njia nyingine. Mchungaji mwema, halisi atalifuatilia kundi hilo lililojitenga, (Kufanya nini?) kuwarudisha. Mchungaji halisi, wa kweli, anafanya nini? Atatangatanga, yeye mwenyewe, (Afanye nini?) awarudishe waliopotea. Anafanya nini? Anaakisi sura ya Mchungaji mwema, akijaribu kurudisha mtu huyo. Ingawa, walienda kombo mahali fulani, ndugu, kana kwamba wangesambaratisha ulimwengu, mara moja. Mchungaji huyo ataenda moja kwa moja, ili kuwaweka sawa, awarudishe moja kwa moja upande huu tena. Huyo ni mchungaji mwema. Anaakisi sura ya Yesu.

95 Ndugu, najua inaitwa uzushi. Inaitwa ulokole. Lakini kama ningekuwa na chaguo la kufanya, usiku wa leo, chaguo langu lingekuwa ni kuwa kama Yeye. Ninataka, vyovyote maishani mwangu, kuakisi sura ya Bwana Yesu, maishani mwangu.

96 Ninaenda, baada ya kesho usiku, baada ya arusi hii, ninaenda nyikani. Ninakusudia kubaki kule, kwa sababu, chini kabisa nafsini mwangu, ninajisikia ya kwamba ninahitaji kutembea kwa karibu na Mungu, kuliko nilivyo. Sitaki kutembea tu. Ninajaribu kutembea sawa, mbele Zake, lakini na—nataka kutembea kwa karibu pamoja Naye. Wakati Maskani ya Branham ikiwa na uamsho, nataka mmoja, mimi mwenyewe. Sitaki tu ufanyike jengoni. Nataka ufanyike ndani yangu. Nataka kutembea kwa karibu. Ninamtaka Roho Mtakatifu kwa zaidi ndani yangu, kumwakisi Kristo ndani yangu. Ninataka kuwa kama Yeye. Najua kwamba kila Mkristo wa kweli—wa kweli anataka kuwa kama Yeye. Hiyo ndiyo shauku ya moyo wangu, kuwa kama Yesu. Yeye . . . Mbona, nataka Yeye awe ninii wangu . . . Nataka Yeye awe ninii . . . Yeye ndiye mfano wa kile ninachotaka kuwa.

97 Basi, tazama, itamhitaji Roho Mtakatifu kufanya jambo hilo. Hicho ndicho kitu pekee kinachoweza kufanya hivyo. Sipendezwi na seminari na yale mtu fulani aliyo nayo ya kuniambia. Sijali kuhusu kubusu msalaba, au kuivuta moyoni mwako, wala kuomba dua kwa wafu. Ninavutiwa na jambo moja, hilo ni, Roho Mtakatifu kwa zaidi kumtawala William Branham. Sivutiwi na kujiunga na kanisa kubwa kuliko nililojiunga nalo. Mimi ni mshiriki wa Kanisa halisi la Mungu aliye hai, Mzaliwa wa Kwanza. Nilizaliwa ndani Yake. Nami nataka Roho Mtakatifu kwa zaidi maishani mwangu, kumwakisi Kristo Ambaye ninampenda. Sijali ni ubapa gani au kiwango gani ninachopaswa kuingia, ili kumpata. Sijali kama itanibidi kwenda *hapa* au kwenda *kule*, niitwe "mlokole, mtakatifu anayejibingirisha," chochote kile. Ninataka Maisha Yake yaakisiwe zaidi. Sivutiwi na ubapa ninaopaswa kuufikia. Ninavutiwa na Roho Mtakatifu, ili niweze kuwa mtumishi zaidi kama Yeye alivyokuwa. Alikuwa Mtumishi wa Bwana. Kamwe hakuja kutumikiwa, ama kutumika, kamwe hakuja

apate kutumikiwa. Lakini, kutumikia, Yeye alichukua mahali pa mtumishi.

98 Na kama Mfalme wa Mbinguni angeweza kufanya hivyo, na sisi ni viungo vya Mwili Wake, hebu sote tuwe vivyo hivyo; sio kuwa tofauti, bali tujinyenyekeze Mbele Zake. Haidhuru ulimwengu unataka kusema nini, ama watu wenye akili, usiliwazie hilo. Pokea tu Roho Mtakatifu kwa zaidi, na uwe kama Yesu. Mnyenyekevu, mpole, mvumilivu, chukua mahali Pake, Naye atachukua pako kwenye ile Hukumu.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

99 Je, ningeweza kuona, usiku wa leo, kundi la mikono katika jengo hili, la washiriki wa kanisa hili na makanisa mengine? Ninaposema, "kanisa hili," namaanisha tu . . . Kuna Kanisa moja tu, hilo ni Kanisa la Mzaliwa upya, Kanisa la Mzaliwa wa Kwanza, Kanisa la Yesu Kristo, wasiozaliwa na ulimwengu, bali wamezaliwa kwa Roho wa Mungu. Ningeweza kuona lundo la mikono ikiinuliwa, na kusema, "Mungu, nifanye kama Yesu. Nifinyange, Ee Bwana. Unioshe, Ee Mungu"? Mungu aibariki mioyo yenu. "Unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji."

100 "Bwana, kuna dosari ndogo na mipindo katika maisha yangu. Nimekuwa nimeketi, nikimsikiliza Ndugu Parnell, na Ndugu—Ndugu Neville na wahudumu wengine wazuri, na Ndugu Collins na wengi wa hao ndugu wanaohubiri. Nimekuwa nikisikiliza. Lakini, Bwana, usiku wa leo, nimefikia tu uamuzi huu: Wananiambia nini? Wanajaribu kunielezea nini? Ninaona kwamba wanajaribu kunifanya niwe kama Yesu. Wala hakuna njia kwangu kufanya hivyo. Mimi—mimi ni chui. Nina madoadoa, na, nikiyalamba, ninayafanya tu kuwa meupe zaidi. Yanakuwa dhahiri tu zaidi kwa ulimwengu. Bwana, nijalie nijipoteze. Sijali inaonekana ni mchafuko wa namna gani, kwa ulimwengu. Ninataka nizaliwe mara ya pili, kwa Roho wa Mungu. Nami nakutaka Wewe, Bwana, unijaze, usiku wa leo, na Roho Wako Mtakatifu. Nioshe. Nitakase. Chukua Damu ya Yesu, unitakase, unisafishe. Kisha unijaze, mpaka nipoteze nafsi, na niipate, Bwana, ndani Yako."

101 Ee Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, uliyemfufua tena Bwana Yesu katika wafu, ukamfufua kwa Roho wa Milele wa Mungu ahuishaye, ukaufufua mwili huo uliokaa ndani yake, na umeuinua mpaka kwenye Kiti cha Enzi cha Mbinguni.

102 Alikuja kwa aliye duni sana duniani, yule kahaba, na akawa mtumishi aliye wa chini kuliko wote, akaenda kwenye mji duni kuliko yote, akashughulika na watu duni sana, akapokea jina duni kuliko yote, na akawa maskini hohehahe. Hata kwa maumbile, "Ndege wana viota, na mbweha walikuwa na matundu, lakini Mwana wa Adamu hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake."

103 Na, hata hivyo, huyo Roho anayehuisha Ambaye alimheshimu Mtumishi huyo wa kweli aliyejifanya Mwenyewe mtumishi, tupate kuwa na mfano wa kufuata, alimfufua kutoka kwenye mashimo ya kuzimu, yaliyoletwa na kaburi. Kisha akaufufua mwili huo, na kuuweka katika Mbingu za mbingu, hata ameinuliwa juu sana hata inamlazimu kutazama chini apate kuziona mbingu. Kisha akampa Jina lipitalo kila jina linalotajwa, mbinguni na duniani pia.

104 Bwana, jalia tumpokee Roho Wake, usiku wa leo. Jalia hiyo iwe ndiyo njaa ya kila moyo humu ndani. Umeona mikono iliyoinuliwa, Bwana, sio kukariri kanuni za imani, wala kujiunga na makanisa, au—au kuyabishania mambo *haya*, au *yale*, bali tuwe wanyenyekevu mioyoni mwetu, tupate kufananishwa na sura ya Mungu. Jalia lifanywe na Roho Mtakatifu, Bwana. Jalia Roho Mtakatifu wa Mungu atufinyange. Sio kwa dhana ya kiakili, kwamba, "Tunapaswa kuwa, na tutafanya hivyo," lakini, huyo ni mtoto aliyeasiliwa. Lakini, Bwana, jalia kweli litendeke kwa Roho Mtakatifu, na Kuzaliwa upya kunakotugeuza, kwa kufanywa upya. . .kwa roho zetu, kutufanya kama Yeye.

105 Yasikie maombi yangu, Bwana. Ni dhaifu. Najua, Bwana, ni dhaifu. Sio kwamba tu ninawaombea wale walioinua mikono yao, lakini kwa mikono yangu mwenyewe iliyoinuliwa juu. Nifanye kama Yeye. Mungu, haidhuru itakubidi kunifanyia nini, ni ubapa gani ninaopaswa kupanda, nifanye kama Yeye. Nataka kuwa kama Yesu, moyoni mwangu. Nijalie, Bwana. Wala si mimi tu, bali wafanye hawa wote hapa, usiku wa leo, hivyo. Tujalie, Baba, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

106 Ufuasi wa kanisa ni sawa. Sina chochote dhidi yake wala lolote la mambo hayo. Lakini, ndugu, kuwa Mkristo, kunamaanisha kufananishwa na sura ya Kristo. Tunataka kuwa sura zilizo hai; si kubeba sanamu, lakini kuwa sura ya Bwana Yesu.

107 Kuna wimbo mdogo ambao nataka mnisaidie kuuimba sasa hivi. Sijui. Siwezi kuuimba, lakini nina hakika nyote mnaweza. Nisaidieni. *Kuwa Kama Yesu*. Ni wangapi wamewahi kuusikia? Ninajua sote tunataka kuwa hivyo, kwa hiyo hebu na tumwimbie.

108 Ninajua ya kwamba Roho Mtakatifu mkuu yuko hapa. Usingeweza kujificha. Daudi alisema, "Nikifanya kuzimu kitanda changu, hata hivyo Yeye atakuwepo huko." Naye atakuwa kila mahali. Kwa hiyo, Yeye yuko papa hapa, usiku wa leo. Anajua kila hatua, kila tendo, kila kitu tunachofanya, kila sura, kila wazo. Anajua yote kulihusu. Je, hamuamini hilo?

> Kwa hivyo kuwa kama Yesu, kuwa kama Yesu,
> Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;

Kote katika safari ya maisha toka duniani hadi
Utukufuni
Naomba tu kuwa kama Yeye.

109 Hivi hamuupendi huo? Sikilizeni hii sasa:

Kutoka hori la Bethlehemu alikuja Mgeni,
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maisha toka duniani hadi
Utukufuni
Naomba tu kuwa kama Yeye.

110 Mnajua kinachorudi mawazoni mwangu sasa hivi? Jana, nilichukua daftari la kale la kanisa. Imekuwa... sijaliona. Vema, kusema kweli, ni mara ya kwanza niliyowahi kuliangalia. Ilinibidi kulitumia wakati kanisa lilipozinduliwa. Na kulikuwako na jina la Ndugu Seward mle, na kulikuwako na Ndugu George DeArk, na Ndugu Weber, majina hayo yote humo. Nikaona pale chini, maskini yale madarasa ya shule ya Jumapili. Nikaona jumla ya matoleo yetu, ya madarasa matano, ilikuwa dola moja na senti sitini, ya maskani hii, kukiweko na mamia walioketi hapa; dola moja na senti sitini. Mnaona? Kisha nikaangalia chati ya siku hizi. Nikawazia, "Ni wangapi wametuacha!" Nilimwona Ndugu Frank Broy pale, ma. Huyo ni baba mkwe wangu. Nikawaona hao wazee wote wa zamani, Bibi Weber. Hao watu wote wa kale, wote wameipanda ile ngazi, wakapanda Juu. Wote wametuacha. Nakumbuka tulipozoea kusimama hapa. Nami nikawazia, "Bwana Mungu, kanisa letu linaweza kuonekana bora zaidi, na tunatarajia kujenga moja, lakini, Bwana, je, unatupenda zaidi sasa kuliko vile ulivyotupenda wakati ule?" Hapana, siamini hivyo.

111 Tulipokuwa tukisimama na kuimba, "Ninatamani tu kuwa kama Yeye, kote katika safari ya maisha." Ninaweza kumwona maskini mzee George huku ukosi umefunguliwa namna *hiyo*, akitokwa na jasho, akikunja leso yake katikati ya vidole vyake. Ninaweza kuona nyuso hizo za watakatifu wapendwa huko nyuma, wakilia, huku wameinua mikono yao.

112 Wahubiri waliingia jengoni wakasema, "Hei, jamani! Unawaweka watu katika nia moja namna hiyo kwa njia gani?"

113 Nikasema, "Sina uhusiano wowote nayo. Walifanywa na kugeuzwa kuwa sura ya Mungu, huko chini kwenye benchi la vumbi la mbao, chini huko mahali fulani, ambapo walimpata Kristo moyoni mwao."

114 Ni harufu nzuri jinsi gani, maombi hayo, yalipokuwa yakipanda juu, sikuzote, usiku kucha. Wakati mwingine tungeingia, na kutembeleana nyumbani, kisha tunaenda nyumbani kwenye mapambazuko; tunaomba usiku kucha. Hatuuoni uaminifu huo tena. Inaonekana kana kwamba wote umetoweka. Kuna nini? Kuna nini? Hebu tuurudie upendo wa kwanza tuliokuwa nao.

Na tuwe tu kama Yesu, kuwa kama Yesu,
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maisha toka duniani hadi
  Utukufuni
Naomba tu kuwa kama Yeye.

115 Mngeomba kweli? Hebu tuuimbe huku mumeinua mikono yenu.

Kuwa tu kama Yesu, kuwa kama Yesu,
  (Kubadilishwa kuwa sura Yake!)
Kwenye . . .

Pendaneni.

. . . kuwa kama . . .

Sisi ni viungo vya Mwili Wake. Ni lazima tuwe kama Yeye.

Kote katika safari ya maisha toka duniani hadi
  Utukufuni
Naomba tu kuwa kama Yeye.

116 Mnamaanisha hilo kweli? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa hiyo si ni roho tamu? Ningependelea kuwa nayo kuliko chochote nikijuacho ulimwenguni. Ni . . . Unaweza kuchukua ulimwengu mwingine wote, na madoido yake, wasomi wako wote, madaktari wako wote, marabi, maaskofu, baba watakatifu. Nipe Yesu. Hiyo ni kweli. Hebu nimpate tu, ile njia ya mtindo wa kale. Ninamhisi ndani kabisa moyoni mwangu, na kutazama maisha yangu, na kuona shauku zangu ni kumtumikia Yeye, mnyenyekevu, mpole na mwaminifu. Hilo ndilo tunalohitaji, marafiki. Ni uhu-. . . Huyo ndiye Yesu. Huyo ndiye Yesu wa Biblia. Sio Yesu wa kiakili, bali Yesu wa nafsi. Yuko hapa, usiku wa leo.

117 Ni wangapi walio wagonjwa na wahitaji? Inueni mikono yenu, unamhitaji Kristo. Wewe ni mgonjwa na unataka kuombewa? Inua mikono yako, juu, ili niweze kuona wewe ni nani.

118 Vema, ni wangapi walio na shauku moyoni mwao, ya kumwombea mtu mwingine ambaye ni mgonjwa? Hebu tuone mikono yenu ikiinuliwa. Vema. Wapo wengi tu.

Ni wangapi wanaoamini kwamba Yesu angali ni yeye yule?

119 Hatuna kadi za maombi zilizosambazwa. Sininii . . . Hakuna kadi za maombi, sivyo? Sidhani walikuwa humu.

120 Je, mnaamini ya kwamba Yesu Mwokozi wetu anaweza kuja, usiku wa leo, kwetu? Na kama tukiimba, nami nikizungumza juu ya kuakisi sura Yake, Yeye angefanya nini kama alisimama hapa? Unafikiri angefanya kama alivyofanya katika Yohana 4, ambapo alimwona yule mwanamke kisimani, na kumwambia, akajua yaliyokuwa moyoni mwake, na kumwelezea, na kumwambia? Naye alijua Yeye alikuwa ni Masihi. Mnaamini

hilo? Mnamwamini Yesu yuyo huyo aliye—aliye Kuhani Mkuu . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.—Mh.] . . . mkono wa Mungu. Unamwamini Yesu yuyo huyo, usiku wa leo, ambaye alikuwa akitembea siku moja . . .

121 Wala hapakuwapo na mstari wa maombi, bali kulikuwako na maskini mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu. Alipenya katikati ya umati mpaka akagusa vazi Lake, akarudi na kuketi. Ndipo Yesu akageuka akasema, "Ni nani aliyenigusa?" Je, mnaamini kwamba Yesu angali ni Yesu yeye yule leo? Na shauku yake, moyoni mwake! Mnaona, aliogopa. Alirudi na kuketi. Alisubiri. Ndipo Yesu akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

122 Ndipo ninii—ninii . . . Petro, mtume, akamkemea, akasema, "Bwana, mbona, kila mtu anakugusa!"

123 Akasema, "Naam. Lakini huu ulikuwa mguso tofauti. Nguvu zilinitoka. Ni—niliuhisi." Naye akatazama pande zote, kwenye kusanyiko, mpaka akamwona maskini mwanamke yule. Naye akamwambia kwamba alikuwa akitokwa na damu na imani yake ilikuwa imemponya.

124 Je, huyo ndiye yule Yesu? Hivi . . . Tungeweza kujinyenyekeza, usiku wa leo, na kubadilishwa kwa kufanywa upya roho zetu, na Roho Mtakatifu, tupate kutoa midomo yetu, macho yetu, na imani yenu, na imani yangu, hata angekuja kwenye hili kusanyiko na kutenda kazi ndani yenu, na kutenda kazi ndani yangu, kulitimiza Neno Lake, kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu? Ameketi mkono wa kuume wa Mungu, kufanya maombezi tunapoungama. Yeye pia ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa jinsi ile ile Yeye alivyoguswa alipokuwa hapa duniani, na mambo ya udhaifu wetu. Je, mnaamini hilo? ["Amina."] Yesu yule yule.

125 Ni wangapi humu ndani walio na haja ya nafsi yako au ya mtu mwingine, baadhi yenu ambao siwajui, mtu ambaye mnajua kwamba sijui hilo? Nitalisema hivyo. Sijui chochote kukuhusu wewe au haja yako. Lakini unaamini ya kwamba Yesu yuko hapa kujifananisha Mwenyewe, kujifanya Mwenyewe aonekane kwetu, kutenda ndani yetu jinsi alivyotenda alipokuwa ndani ya Yesu Kristo. Je, unaamini hayo? Inua mikono yako, yeyote kati yenu ambaye unajua sikujui sasa. Unaona? Sikujui.

126 Vema, hebu tuone. Tunaweza kuzingatia wapi, mara ya kwanza? Sasa iweni na kicho. Kama atafanya hivi, utamwamini, kwa moyo wako wote? Unaona? Ninajisikia tu . . . Nilikuwa nikitaka kuwaita hapa juu na kuwawekea mikono. Siamini nitafanya hivyo. Ninaamini Yesu yuko hapa.

127 Sisi, sio—sio kubeba sanamu Yake, bali kuwa mfano Wake. Huyo ndiye Yesu tunayemtaka. Sivyo? Kuwa mfano! Vema.

128 Sasa, Bwana Mungu, hii hapa taarifa kuu. Bali ni Wewe, Bwana, uliyetoa hiyo ahadi. Sasa inatupasa kusonga mbele. Sasa jambo fulani halina budi kutendeka, ingawa sisi hata si

madhehebu. Sisi ni maskini kundi dogo tu nyenyekevu la watu waliofunikwa, hata, wengi wetu tungefukuzwa kutoka katika makanisa makubwa ya kielimu. Kama tungeenda, tusingeweza kuvaa mavazi kama walivyofanya. Halafu, jambo jingine, kama tungesimama, na Roho angebariki na tungesema, "Amina," kama Maandiko yasemavyo, tungetolewa nje, mara moja. Na wengi hawangepokelewa: baadhi yao, kwa sababu ya rangi yao; baadhi yao, kwa sababu ya kanuni yao ya imani; baadhi yao, kwa sababu ati wanakupenda Wewe sana. Na wa—wana Roho. Wamekufa kwa mambo ya ulimwengu, na wamezaliwa upya. Lakini wanao Uzima mpya, Uzima wa mtumishi.

129 Lakini tumekusanyika hapa, Bwana, chini ya paa hili dogo ambalo Wewe umetupatia, ambalo tunathamini. Sasa, Bwana, jalia ijulikane ya kwamba Wewe ndiwe Kristo, yeye yule, na ya kwamba huyu Mkuu tunayenena habari zake, Yeye yupo sasa kujulisha na kufanya kama vile Yeye alivyofanya alipokuwa hapa duniani. Jalia, Baba, wapate kuona na kuamini. Kwa maana ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

130 Je, unaamini kwamba, unachoomba, unapata? Imani ni nini? Imani ni ukweli. Imani ni kitu ambacho unajua hakika. Imani si kitu unachobahatisha. Imani ni kile unachojua, unaona, kitu kinachoshuka nafsini mwako.

131 Natamani wale ambao hawanijui, nami siwajui, na bado una haja au shauku, naomba mwinue mikono yenu tena. Nataka tu kupata wa—wazo la kijumla, kila mtu hapa ndani nisiyemjua. Vema. Ni kila mahali tu. Sipendi kuongea na watu ninaowajua, kwa sababu wengine wangesema, "Anawajua." Lakini kuna mikono mingi iliyoinuliwa, ambao sikuwajua. Sasa, kama Bwana Yesu atalijalia hili, je, ninyi wengine mtaamini kwa moyo wenu wote, na kukubali uponyaji wenu na chochote kile?

132 Tafadhalini, na—na tuninii, mioyoni mwetu, tuombe "Yesu ondolea mbali mashaka yote." Mbona, Yesu hawezi kutilia shaka. Ikiwa tuko katika mfano Wake, tunaamini. Yeye alimwamini Mungu. Alikuja kufanya mapenzi ya Mungu. Hakujali kile mwanadamu alichosema, ama mtu mwingine alichosema. Alikuja kufanya jambo moja: kuwa mtumishi wa Baba Yake. Naye Baba Yake alikaa ndani Yake. Tunakuja kuwa mtumishi wa Mungu. Roho Mtakatifu anakaa ndani yetu. Tunataka kumtumikia.

133 Nitamzingatia mwanamke mmoja, mwa—mwanamke mweusi aliyeketi moja kwa moja hapa nyuma. Ninaamini aliinua mikono yake, kwamba sikumjua. Kwa kuwa—kuwa . . . Vema, kuna wawili wao pale. Vema. Hakuna mmoja wenu kina mama anayenifahamu, au ninayemfahamu? Kama hiyo ni kweli, inueni mikono yenu, ya kwamba siwajui. Inueni mikono yenu. Vema. Vema. Hatufahamiani. Katika Maandiko, ilinenwa . . . Sababu ya mimi kuwaona, ninyi ni . . . Mlikuwa watu weusi. Mnaona?

134 Kulikuwa na mwanamke, wakati mmoja, katika Biblia, mlango wa 4 wa Yohana Mtakatifu. Yesu alikuja karibu na kisima, na palikuwa na mwanamke Msamaria. Alikuwa mwa—mwanamke wa jamii nyingine. Ndipo Yesu akazungumza naye, dakika chache tu, mpaka akapata kujua shida yake ilikuwa nini, na kumwambia shida yake ilikuwa ni nini. Basi alipomwambia shida yake, akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Sasa, tunajua, Masihi ajapo, Yeye atatuambia mambo haya." Lakini hawakuelewa Yeye alikuwa ni nani. "Mbona," akamwambia, "u nani Wewe?"

Ndipo Yesu akasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye."

135 Akarudi mjini, alikotoka, na kusema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya, akaniambia kuna shida gani. Haimkini huyo kuwa ndiye Masihi?"

136 Je, ninyi wanawake mliwahi kusoma hayo? Hakika. Yohana Mtakatifu, mlango wa 4. Naam, kama. . . Yesu ni yeye yule jana, leo na hata milele. Nawe umesimama yadi ishirini kutoka kwangu, ama umeketi, hasa. Je, unaamini ya kwamba Yesu yeye yule, akinena kati yetu, angeweza kunifunulia utakacho, kutoka hapa? Kama nimewaambia Kweli, kwa kuwa Biblia hii ni kweli, Yeye anaweza kufanya hivyo, sivyo? Kama atafanya hivyo, mtaamini?

137 Huyo mwanamke hapo mwishoni, akinitazama, *hivi*, anasumbuliwa na ugonjwa wa mgongo ambao anataka aponywe kutokana nao. Hiyo ni kweli kabisa. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mama uliye hapo mwisho. Haya basi.

138 Sasa vipi kuhusu wewe, mama? Je, unaamini, pia? Ninaamini ulisema hatufahamiani, pia, karibu naye. Una matatizo ya kichwa chako. Na una tatizo la ngozi, pia. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

139 Sasa, nendeni nyumbani. Nyote wawili mnaweza kuwa wazima. Imani yenu imewaponya.

140 Je, mnaamini ya kwamba Yesu yuko hapa, usiku wa leo? Vipi kuhusu baadhi yenu, wengine jengoni? Mahali pengine, amininі.

141 Huyu hapa mwanamke ameketi hapa, akiomba. Yeye ni shujaa. Ninamjua, lakini siwezi kujizuia kwa kuwa hiyo Nuru inaning'inia juu yake. Huyo ni Binti Bruce. Sasa, Binti Bruce, sijui lolote kuhusu tatizo lako. Uliponywa, kansa, wakati mmoja. Lakini papo hapo kwenye mlango huo, mara ya kwanza nilipowahi kuuza. . . kukwambia. . . nilipopata kukuona umesimama kwenye mlango huo, Roho Mtakatifu aliniambia jambo ambalo hakuna mtu anayejua mbali na wewe na daktari. Hiyo ni kweli. Sivyo? Je, unaamini anaweza kuniambia tatizo ni lipi sasa? Ninakufahamu, ila si—sijui shida yako ni nini. Sina habari. Hakika, umeponywa ile kansa. Lakini siwezi kuiepuka hiyo Nuru inayoning'inia juu yako. Unaona? Imekaa papo hapo.

142 Sasa, naona mtu mwingine akiinuka. Sio kwa ajili yako. Ni kwa ajili ya mtu fulani aliye na kansa. Hiyo ni kweli kabisa. Halafu ninamwona mwanamke, ama kitu fulani. Yeye ni mwenye dhambi, ama kitu fulani, ana mazoea ya kunywa pombe, ama kitu fulani. Nawe umebeba leso mbili, nipate kuziwekea mikono yangu, kwa ajili ya—ya ukombozi wao. Hilo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa wewe kuwa mwamuzi. Je, hiyo ni kweli? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

143 Mtu fulani nyuma *hapa* ndani, ambaye simjui, inua mkono wako, mtu ambaye simjui. Hapa, kuna. . . Hiyo ni nini? Inua mikono yako tena, papo hapo pembeni. Kuna wanawake wanne ama watano wameketi pale. Je, mnaniamini mimi kuwa mtumishi Wake? Je, mnaamini kwamba kile mnachokiona kinaendeshwa na Roho wa Mungu? Mnaamini? Ikiwa unaweza kuamini.

144 Mwanamke anayeketi, akiniangalia, amevaa kofia ndogo, amevaa miwani, hereni nyeupe. Naam. Sio kwa nafsi yako. Ni kwa ajili ya mtu mwingine, nao ni mahututi. Ni kutokwa damu kwa ndani. Wako hospitalini. Hospitali hiyo ni New Albany. Hiyo ni kweli. ROHO MTAKATIFU ASEMA HIVI.

145 Huyo msichana, je, uliinua mkono wako? Yule mwanamke, upande *huu* mwingine, akinitazama hivi, unaniamini? Una shauku moyoni mwako. Unaamini ya kwamba Mungu angeweza kunifunulia? Vema. Unamwombea mtu mwingine, pia. Ni mtu aliye na watoto wa macho machoni mwao. Wanahofu watakuwa vipofu. Hiyo ni kweli. Sasa, kama utaamini kwa ajili yake, hataingia upofu kama utaamini.

146 Mwanamke huyo moja kwa moja nyuma, pale mwishoni, nyuma ya yule mwanamke aliyeinua mkono wake. Una tatizo la neva. Hiyo ni kweli. Wasiwasi wako uko kwenye koo lako. Hiyo ni kweli. Sivyo? Basi inua mikono yako kama mambo hayo ni kweli. Ninyi wanawake hapo, ninazungumza. Vema.

147 Huyo mwanamke mwingine alikuwa ni yupi pale? Je, ni wewe uliyeinua mkono wako, pia, dada, hapo? Inua mkono wako, huyo mzee. . . Vema. Una ugonjwa wa baridi yabisi unaotaka uombewe. Hiyo ni kweli. Sivyo? Inua mkono wako. Unaamini?

148 Mtu fulani—mtu fulani nyuma ya kanisa, amini, uwe na imani.

149 Ninamwona mwanamke akinitazama moja kwa moja, anaangalia kati ya wanawake wawili papa hapa. Ameinua kidole chake kinywani mwake. Anakabiliwa na upasuaji, wa kidole tumbo. Hiyo ni kweli kabisa. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mama. Huyo hapo.

150 Unaamini? Ni kitu gani? Ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Je, unaamini kwa moyo wako wote?

Sasa, hebu kidogo, dada.

Kuwa kama Yesu, kuwa kama Yesu,
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maisha toka duniani hadi
  Utukufuni
Naomba tu kuwa kama Yeye.

151 Sasa unakuona kule kufa kwa kanisa la siku hizi. Ni nini kingetukia katika siku za Bwana Yesu, wakati lilipotukia? Mwanamke huyo, alifurahi sana, akaangusha mtungi huo wa maji, naye huyo akakimbia mjini. Akasema, "Masihi yuko hapa!" Lakini, siku hizi, naam, hujapata mchafuko wa kutosha, pale madhabahuni, kupokea Kuzaliwa upya bado. Kuna kasoro mahali fulani. Hiyo ingemtuma Roho Mtakatifu kupitia mahali hapa, ingeanzisha uamsho, uakisi wa Yesu Kristo, sura Yake ikifananishwa hapa, akitembea miongoni mwa watu, kufanya jambo hilo. Kuna shida gani? Kuna kasoro fulani. Tunahitaji uamsho.

152 Je, ni wengine wangapi walio wagonjwa? Inueni mikono yenu, mlio wagonjwa na wahitaji.

153 Wekeaneni mikono. Na tuombe. Upesi sana sasa, wekeaneni mikono, iweni tayari kupokea uponyaji wenu. Kama utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kuponywa sasa hivi.

154 Nilishangaa. Tulikuwa tukizungumza juu ya mwanamke, kuzaa. Bado sijapata, maishani mwangu, kuwa na mwanamke mmoja, nijuavyo mimi, aliyewahi kuja jukwaani, akitamani kupata mtoto. . .Nini kinatokea? Kama ningeweza kumwona, na kuona ikitendeka, shauku yake ya kutaka kitu kifaacho, ninamwambia, "Mama, unatafuta mtoto."

Yeye, "Ndiyo, Ndugu Branham."

155 Ninamjua mwanamke, mwenye umri wa miaka arobaini na tisa, aliye na mtoto mchanga wa kiume sasa. Maisha yake yote, aliishi na mwanamume huyu tangu, vema, tangu akiwa na yapata umri wa miaka kumi na sita. Yeye ana arobaini na tisa, mumewe hamsini na kitu. Mara tu iliposemwa, "BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli, utampata mtoto huyu." Alienda nyumbani na kununua nguo za mtoto. Miaka mitatu baadaye, akiwa na umri wa miaka hamsini na miwili, akajifungua mtoto mvulana ambaye alitamani kumpata. Kwa nini? Aliposikia likinenwa, alijua ilibidi litimie. Ilifanya nini? Ilimweka katika mtazamo unaofaa. Kama hawa . . . Roho Mtakatifu ni mzuri sana kuja na kusema mambo haya kwa watu. Ikiwa ataninii . . . Ikiwa utaingia katika mtazamo mzuri sasa, uponyaji umekamilika.

156 Ee Bwana, Wewe ni Mungu, na Wewe ni Mungu hata milele. Nasi tu—tuna furaha sana kujua ya kwamba uliahidi ya kwamba ungekuwa na masalia wakati utakapokuja duniani. Haijalishi kijacho wala kiendacho, kutakuwako na watu fulani watakaokuwa tayari. Tunajua kwamba kuna fungu la kumi ambalo mwanadamu humtolea Mungu. Na kuna fungu la kumi

miongoni mwa watu. Pengine, labda tungesema, fungu la kumi, la mavuno yote ya ulimwengu kote katika nyakati, watakuwa ni Wateule ambao wameitwa.

157 Ee Baba, tunaomba, tunapofanya kazi hapa, sisi sote pamoja, tukitafuta-tafuta mjini, tukijaribu kuwaingiza wenye dhambi, tukijaribu kufanya jambo fulani kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Tunashuka mjini, tunakutazama kule kutojali. Tunakuona. Na kama vile Lutu, kule Sodoma, inazitesa nafsi zetu kila siku, kuona wanawake wakivuta sigara na—na kujidai kuwa ni Wakristo, na kunywa, na kufanya karamu, na kuvaa nguo zinifu. Na—na wanaume wakishikwa na tamaa mbaya. Na, loo, dhambi ya Sodoma! Mioyo yetu inahuzunika ndani yetu, Bwana.

158 Loo, si ajabu imani imeshuka chini sana, wakati watu wako hivyo, wanaikosa Damu ya Yesu. Hiyo ingezitakasa nafsi zao na kuwatia moto kwa ajili ya Mungu, hata hivyo hawataipokea. Nayo ile misheni ndogo pembeni, ya kupiga matari na ngoma, iko pembeni mwao, na wanatucheka tukiwaleta watakatifu wa Mungu aliye hai.

159 Loo, jinsi tunavyokushukuru Wewe, Baba, kwa ajili ya ubapa fulani, mahali fulani, ambao utahubiri Injili, ambao utawanyooshea watu mikono. Tujalie, Bwana, sasa hivi tunapoomba, na kujua ya kwamba Roho Wako Mtakatifu mkuu na Malaika wako—wako mahali pao humu kanisani.

Mungu, samehe kila dhambi.

160 Watu ni wagonjwa hapa, usiku wa leo. Kuna wengi wao. Umejionyesha Mwenyewe kuwa uko hapa, Bwana, kupitia watumishi Wako. Wengi wao huko nje waliokuwa wakifikia na kuita na kuvuta. Pia, Bwana, unajua ya kwamba—ya kwamba Wewe Ndiwe pekee Ambaye ungeweza kuruhusu hili lifanyike. Wewe ni Mungu, na Mungu pekee, Nawe unalifanya kwa kusudi lile lile uliloahidi ya kwamba ungelifanya. Nayo ndiyo ishara ya mwisho kwa kanisa, kama ulivyonena. Wakati wa mwisho umewadia.

161 Ndipo ukauliza swali hili, "Je, nitapata imani nitakapokuja duniani?" Kamwe hukuuliza, "Je, nitapata wafuasi wa kanisa? Je, nitapata kanuni za imani? Je, nitapata uaminifu?" Ulisema, "Je, nitapata imani nitakapokuja duniani?"

162 Bwana, jalia watu hawa wagonjwa waachilie imani yao, watoke kwenye vurugu, na mashaka, na woga. Imani yao na ifunguliwe sasa hivi. Na kama wakiiachilia imani yao, itabidi ugonjwa uachilie, ibilisi atawaachilia, nao watawekwa huru kwa Nguvu za Mwenyezi Mungu. Roho Mtakatifu na aloweshe kila moyo, aibatize kila nafsi, na kuponya kila mwili ulio katika Uwepo wa Kiungu. Tujalie, Bwana.

163 Kwa ajili ya hili ninaomba, ya kwamba ibilisi amwache kila mtu wanayemtesa humu, usiku wa leo. Katika Jina la Yesu

Kristo, Shetani, jiondoshe kwa watu hawa. Kama mtumishi wa Mungu, ninalia kwa niaba yao, nikiwaombea rehema. Amina.

164 Ni wangapi wanaoamini kwa moyo wenu wote sasa, kwa yote yaliyo ndani yenu, kwamba Yesu Kristo anajiakisi Mwenyewe duniani leo miongoni mwa watu Wake? Je, mnampenda?

165 Basi na tuimbe wimbo huu wa kale pamoja, *Nampenda*. “Nampenda kwani alinipenda kwanza.” Sote pamoja, tunaposimama sasa. Kila mtu sasa, sote pamoja. Ni wangapi wanaoujua? Inueni mikono yenu. *Nampenda*. Hebu tumwabudu sasa.

166 Wagonjwa wote, wote wanaoteseka, simameni kwa miguu yenu sasa, mpokee uponyaji wenu. Ninaamini, na kwa moyo wangu wote. Laiti ungaliiachilia imani yako iende, sasa hivi! Kristo wa Mungu, aliyepo, ataninii . . . Anafanya nini? Akitufanya mfano Wake. Unaona? Roho Wake hapa, akijiakisi Mwenyewe moja kwa moja kwenu.

167 Sasa, mnajua sio mimi. Siwajui watu hao, hata wawe nani, walioinua mikono yao. Waliinua mikono yao, kwamba hawakunijua. Nami nikainua mikono yangu, sikuwajua. Lakini Mungu anawajua. Ni kitu gani?

168 Ni Kristo akijiakisi Mwenyewe. Ni imani yako kuamini. Ni imani yangu kwa huduma, aliyonithibitishia kwa Malaika; ambaye picha Yake mnaiona, inayoning’inia kwenye kumbi za sanaa za kidini, na ambapo iko ulimwenguni kote, inajulikana, ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli.

169 Wakati ilipofanyika mwili, ilikuwa katika umbo lilioitwa Mwana wa Mungu. Alisema, “Nalitoka kwa Mungu na nikaenda kwa Mungu, narudi kwa Mungu.”

170 Baada ya kifo, kuzikwa na kufufuka Kwake, Paulo alikutana Naye, akienda zake Dameski, katika umbo la Nguzo ya Moto, katika Nuru iliyoyapofusha macho yake. Paulo alisema, “U nani Wewe, Bwana?”

171 Akasema, “Mimi ni Yesu. Ni vigumu kwako kuupiga teke mchokoo.”

172 Yesu alisema, “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu,” kosmosi, utaratibu wa ulimwengu, wafuasi wa kanisa, na kadhalika, “hautaniona tena, hata hivyo ninyi mtaniona. Kwa kuwa Mimi,” kiwakilishi nafsi, “Mimi, Yesu yule yule, nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Nyingi kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu.” Amina. Loo, jamani!

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

173 Loo, tunapoimba huo tena, ninataka Wamethodisti, na Wabaptisti, na Wapentekoste, na Wanazarayo, na Pilgrim Holiness, church of God, wote, ninyi nyote pamoja, nataka mpeane mikono na mtu aliye mbele yako, na nyuma yako, na kando yako, tunapofanya hivyo sasa. Sote pamoja.

> Na . . . (Mungu akubariki, ndugu, mchungaji.) . . . mpenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Kalvari . . .

174 Sasa huu ndio utaratibu wa ufufuo, "Sisi tulio hai na tuliosalia hatutawatangulia hao waliokufa, kwa kuwa parapanda ya Mungu italia na waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza. Sisi tulio hai na tuliosalia tutanyakuliwa pamoja nao, kukutana sisi kwa sisi kabla hatujamlaki Yeye. Tutakutana sisi kwa sisi kabla hatujakutana Naye, tunyakuliwe pamoja Naye, pamoja nao, kumlaki Bwana hewani, sote pamoja."

175 Sasa tumekutana, tukapeana mikono, sasa hebu tumwamkue Yeye.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Kalvari . . .

Uimbeni polepole.

176 Msichana mmoja aliondoka papo hapo mstarini, akaja papa hapa na kupiga magoti madhabahuni, akiugua na kulia. Je, wapo wengine hapa wanaohisi ushawishi uo huo, wangependa kupiga magoti pamoja naye? Tungefurahi ukija mara moja hapa na kuchukua nafasi. Mungu akubariki, ndugu. Je, mtu mwingine anaweza kuja moja kwa moja huku? Hilo ni sawa.

> Na . . .

(Nifinyange, Bwana, na unifanye.)

> . . . Na . . .

Shuka kwenye nyumba ya Mfinyanzi. Mtu mwingine anakuja kuchukua nafasi?

> . . . kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

Loo, Yeye si ni wa ajabu?

177 Bwana mbarikiwa, msichana huyu unamjua Wewe. Simjui mimi. Lakini kuna kitu cha kigeni kilichomgusa muda mfupi uliopita, hata akatoka kwenye kusanyiko akaja, bila ushawishi wowote. Huyo alikuwa ni Wewe, Bwana. Amepiga magoti hapa madhabahuni, huku wapendwa walio karibu, wakimkumbatia.

Wakiomba rehema, na mwongozo, na nguvu za kiroho, kwake. Na lifanyike, Bwana. Imeandikwa, sasa na ifanyike, kwamba, "Hutawanyima chochote chema wale waendao kwa unyofu mbele Zako. Ahadi Zako ni ndiyo na amina, kwa wale wote watakaokupenda na kukufuata Wewe."

178 Hebu msichana huyo ajue hili, hakika, usiku wa leo, ya kwamba hakuna kitu Mbinguni, kilichoahidiwa katika Neno la Mungu, ila kwamba Mungu anataka hata na zaidi kukimwaga moja kwa moja moyoni mwake wakati uu huu. Jalia kuwe na fungu kubwa sana la kuridhisha atakalopewa, wakati amepiga magoti akisujudu madhabahuni. Jalia Roho Mtakatifu ampe mambo yale yanayotamanika moyoni mwake. Tujalie, Bwana, kwa kuwa tunaomba haya katika Jina la Yesu.

> . . . alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Pale . . .

(. . .?. . .)

179 Mungu mpendwa, mwanamke huyu na apewe shauku yake, kwa ajili ya mpendwa wake aliyempenda sana. Jalia Roho Mtakatifu mkuu aifanye kazi, ambayo ni Yeye pekee awezaye kuifanya kwa wakati huu. Tunayakabidhi yote Kwako; tunaomba kwamba . . . Fadhili zako ni bora kuliko uhai. Daudi alisema hivyo. "Kwa kuwa fadhili Zako ni bora kwangu kuliko uhai, midomo yangu itakusifu." Mpe shauku ya moyo wake, Bwana.

180 Wakati kanisa hili, pamoja nami, mhudumu Wako, tutaninii . . . na wahudumu wengine walioko humu jengoni, tunaiombea haja yake kwa uaminifu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Tunalidai, dada. Ubarikiwe.

181 Sasa wakati watu hawa wakijiweka wakfu, wakijiweka wakfu, wenyewe, kwa Bwana, wakati Roho Wake anapotembea humu jengoni, ningependa tusimame kwa dakika moja tu. Mchungaji anawashughulikia madhabahuni. Hebu tuwe katika maombi, kwa muda mfupi tu sasa. Anakuja huku. Basi hebu tuwe tukiimba sasa. Anazungumza na kila mmoja.

182 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu, ili tuwe katika maombi.

> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.
>
> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini
Kwamba Yesu ananiokoa sasa.

Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini
Kwamba Yesu ananiokoa sasa.

Nitamkubali kwa Neno Lake,
Nitamkubali kwa Neno Lake.
Ananiletea wokovu bure
Nami nitamkubali kwa Neno Lake.

Ninaweza, nitaamini, nina . . .

183 Angalia hapa, jamaa mdogo. Je, unataka kutembea kwa kina pamoja na Mungu? Unaamini ya kwamba angekupa wewe? [Ndugu huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Kama utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kuupokea. Unaona? Unaamini? ["Naam, bwana. Ninaamini."] Unalikubali? ["Naam, bwana."]

. . . amini kwamba Yesu ananiokoa sasa.

184 Wote wampendao, inueni mikono yenu. Mseme, "Ninampenda, kwa yote—yote yaliyo ndani yangu." Yeye si ni wa ajabu? Tunapoinamisha vichwa vyetu, katika maombi ya kufunga tu . . . Kumbukeni ibada kesho usiku. Nitawaulizeni, hivi . . .

185 Mkipenda sasa, haraka iwezekanavyo, kila mmoja wenu aliyeinua mkono wake kwa ajili ya wokovu, kutembea karibu zaidi, amini umepokea. Ikiwa huwezi kuuhisi, chukua mtoto aliyeasiliwa. Unaona? Endelea kusema unayo hadi iwe halisi.

186 Wewe uliyekubali uponyaji, wala husikii tofauti yoyote; unasema, "I—imani yangu haitoshi kuihamisha sasa hivi, Ndugu Branham."

187 Chukua njia ya mtoto aliyeasiliwa. Endelea tu kusema, "Bwana, nimepona. Ninaiamini." Itakuja. Itakuweka katika hali ifaayo, unaona, na ndipo imani yako itakuwa sawa. Italichukua. Liamini tu kwa moyo wako wote.

188 Sasa, kesho usiku, ibada zitaanza saa moja na nusu, wakati wa kawaida, kesho usiku, na kila usiku juma hili. Njoni mkamsikie Ndugu Neville na wahudumu hawa wengine, na sisi sote, pamoja, tunaojaribu kuleta uamsho. Mungu awabariki. Hatuwezi kuuleta. Hamna budi—hamna budi kuuleta pamoja nasi, kwa kuomba, kuja, kuwepo hapa. Mungu awe nanyi.

189 Sasa, laiti ninyi, mara tu tunapofumukana, upesi uwezavyo, ili . . . mwondoke humu jengoni. Tuna takriban nusu saa ya mazoezi hapa yatakayofanyika. Na baadhi ya hawa watu wanafanya kazi. Nasi tutainamisha vichwa vyetu.

190 Nami naamini nilimsikia Ndugu Junie Jackson nyuma kwenye kusanyiko. Ndugu Junior, uko hapa usiku wa leo? Yule ndugu kutoka New Albany, kanisa la Methodisti. Vema. Ndugu Jackson utaturuhusu tuondoke kwa maombi?

[Ndugu Jackson anaanza kuomba. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .?. . . kuwa kwenye arusi, njoo mbele upesi sasa.

191 Bwana awabariki. Tutawaona kesho usiku.

> Mtoto wa huzuni na wa majonzi;
> Itakupa furaha na faraja.

(. . .?. . .)

Sura Za Kristo SWA59-0525
(Images Of Christ)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumatatu jioni, tarehe 25 Mei, 1959, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org